

## **Kanuni kuhusu mienendo na tabia ya ngono kwa wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu**

Wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu **wanaweza kuadhibiwa na hata kufutwa kazi kwa tabia isiyokubalika inayohusiana na ngono**. Zifuatazo ni kanuni ambazo ni lazima zifuatawe:

- Watumishi wa mashirika ya kibinadamu **hawaruhusiwi kujihusisha na mahusiano ya kingono na mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, hata kama sheria inaruhusu katika nchi yao**. Kusema ya kwamba haukujua umri halisi wa muhusika sio sababu ya kutosha kujitetea
- Watumishi wa mashirika ya kibinadamu **hawaruhusiwi kulipia ngono kwa pesa, kazi, bidhaa au huduma** - hii ni pamoja na kutumia bidhaa na huduma za msaada zinazotolewa kwa watu wenye uhitaji. Pia hawapaswi kutoa ahadi za vitu hivi ili kuwalazimisha watu wakubaliane na tabia za kudhalilisha na kuwatumia kwa aina yoyote. Hii ni pamoja na kulipa au kutoa fedha kwa ajili ya kununua huduma ya kingono kwa wanaofanya biashara ya kuuza miili yao.
- Wafanyakazi wa kibinadamu wana ushawishi kwa watu wanaopokea misaada ya bidhaa na huduma. Hii inawaweka kwenye nafasi kubwa na mamlaka kwa watu wanaohitaji misaada. Kwa sababu hiyo, mashirika ya kibinadamu **yanaweka msisitizo kuhimiza wafanyakazi wasiwe na mahusiano ya kingono na mtu yeyote aliyeathirika** na majanga ya dharura ya kibinadamu. Mahusiano ya aina hii yanafanya shughuli za mashirika ya kibinadamu kuonekana yasiyo adilifu na kuaminika.
- Ikiwa mfanyakazi wa mashirika ya kibinadamu ana **wasiwasi au kuwa na shuku** kwamba kuna mfanyakazi katika shirika lake au shirika lingine la msaada ambaye anawezakuwa anavunja kanuni za mwenendo na tabia za kingono wa mashirika ya kibinadamu, **ana lazimika** kutoa taarifa, kulingana na na **taratibu** zilizowekwa na mashirika yao.
- Wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu **wanapaswa kujenga na kuendeleza mazingira ya kazi** ambayo yanazuia tabia za kingono zisizokubalika na kuwahimiza wafanyakazi kuwa na tabia zinazokubalika kulingana na **kanuni za maadili zilivyoainishwa katika miongozo. Wakurugenzi wote** wana wajibu wa kusaidia na kuendeleza mifumo inayohifadhi mazingira haya.

Kanuni za IASC kuhusu unyanyasaji na ukatili katika uhusiano wa kingono zinapatikana hapa:

[http://www.pseataaskforce.org/uploads/tools/sixcoreprinciplesrelatingtosea\\_iasc\\_english.doc](http://www.pseataaskforce.org/uploads/tools/sixcoreprinciplesrelatingtosea_iasc_english.doc).

Toleo hili la lugha rahisi inayosomeka imetayarishwa kwa ushirikiano kati ya Timu ya Kazi ya IASC kuhusu Uwajibikaji kwa Watu Walioathirika na Shirika La Kupambana na Unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia pamoja na Shirika la Translators without Borders.